

Mhandisi William Christian ana uzoefu wa miaka 26 katika Sekta ya Maji kwenye maeneo ya usimamizi wa utoaji wa huduma ya maji na ujenzi wa miradi ya maji. Amefanya kazi kama Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji ya Mji wa Singida (SUWASA) kwa miaka mitano, pia amekuwa Mkurugenzi wa Miradi ya Maji katika mfuko wa MCA-T (Tawi la Millenium Challenge Cooperation ya Marekani) kwa muda wa miaka minane na Mhandisi Mkazi kwa miezi ishirini wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji wa Tabora chini ya USRP. Kwa kipindi cha miaka nane amefanya kazi katika Wizara ya Maji katika nafasi mbalimbali. Kuanzia Julai, 2018 mpaka leo anaitumikia Wizara ya Maji akiwa Mkurugenzi Msaidizi wa Usanifu na Ujenzi.

Elimu yake ni Shahada ya Uhandisi toka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Shahada ya Uzamili katika Uhandisi wa Rasilimali za Maji toka Chuo cha Catholic University of Leuven na Vrije University Brussels, Ubeljiji, Astashahada ya Haidrolojia toka Chuo cha Vrije cha Brussels, Ubeljiji, pamoja na mafunzo ya vitendo ya mwaka mmoja, nchini Ujerumani. Pia, mwaka mmoja mafunzo ya juu akikobea katika Upangaji, Usimamizi na Kupunguza Upotevu katika Miradi ya Usambazaji Maji na uelewa wa kina katika Usimamizi wa Mikataba (*FIDIC*).